# Orodha ya stadi: Vifaa saidizi vya kupangilia umezaji dawa

| Mshiriki wa Mafunzo: | Mshauri: | Tarehe: |
|---|---|---|

| Vigezo | Ushauri | Ndio | Hapana |
|---|---|---|---|
| **Hatua ya kwanza: Kuchagua** | | | |
| Inaanza kwa kufanya tathmini ya kupata kifaa saidizi cha kupangilia dawa kwa kumuomba mgonjwa kuleta orodha ya dawa na dozi ambazo atameza mara kwa mara. | | | |
| 1. Inahusika na ukusanyaji wa taarifa zinazoendana na kifaa saidizi husika kwa kutumia fomu ya tathmini na fomu hii inaainisha:<br>• kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa<br>• inadodosa kama msaidizi wa mgonjwa yupo iwapo mgonjwa anahitaji usaidizi katika kumeza dawa.<br>• inachagua aina ya kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa ambacho kinamfaa mgonjwa. | | | |
| 2. Inahusisha ukusanyaji taarifa kwa kutumia orodha ya dawa inayohusu dawa zote ambazo mgonjwa anameza mara kwa mara.<br>• Inaelezea lengo la kila dawa katika lugha rahisi<br>• Inaweka kumbukumbu ya idadi ya dawa ambazo mgonjwa anapaswa kumeza kila dozi | | | |
| 3. Inaainisha wakati ambapo mtu anapaswa kupata rufaa kwenda kwenye huduma sahihi. | | | |
| **Hatua ya pili: Fundisha** | | | |
| 4. Inahusu kumfundisha mgonjwa na/au msaidizi wake namna ya kujadawa dawa kwenye kifaa saidizi cha kupangilia umezaji dawa ikiwemo:<br>• Namna ya kutambua kila kidonge<br>• Namna ya kuweka kila dawa kwenye kifaa saidizi. | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. Inahusisha kujadili na/au kumfundisha mgonjwa namna ya kuweka mpango wa mazoea na wakati wa kutumia kifaa saidizi cha kupangilia dawa | | | |
| 6. Inamfundisha mgonjwa namna ya kutunza kifaa saidizi chake cha kupangilia umezaji dawa. | | | |
| **Hatua ya tatu: Ufuatiliaji** | | | |
| 7. Inahusisha kufanya ufuatiliaji wa mambo kama vile:<br>• Kutoa mafunzo zaidi<br>• Kubadili kifaa saidizi<br>• Kutoa rufaa kwenda kwenye huduma nyingine | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kwa hatua zote** | | | |
| Katika hatua zote,onyesha kuwa hatua zote hizi zinamlenga mgonjwa | | | |

## Taarifa kwa wasimamizi

**Tumia orodha ya stadi ili ikusaidie:**

- Kutathmini ni kwa namna gani washiriki wa mafunzo wanatekeleza stadi hizi ili kuweza kugawa vifaa saidizi vya kupangilia umezaji dawa na kama:
  - Wanaweza kugawa vifaa saidizi vya upangiliaji dawa bila ya kuwa na msaada, au
  - Wanahitaji ushauri zaidi na kama ndivyo hivyo, ni stadi zipi wanahitaji kufanyia mazoezi.

**Kumbuka kwamba:**

- Orodha ya dawa inalenga stadi muhimu zaidi ambazo ziko kwenye moduli ya TAP
- Unaweza kuboresha orodha hii kama kwa kufanya hivyo kutasaidia.
- Inawezekana usiweze kuona stadi kwa hatua zote nne kwa mkupuo mmoja, kutakuwepo na ufuatiliaji kwa tarehe itakayopangwa.

**Ili kutumia orodha ya stadi:**

- Angalia kwa makini wakati washiriki wa mafunzo wakifuata hatua za ugawaji wa vifaa saidizi. Hii inawezekana kufanyika kwa igizo ( kati yao) au pamoja na wateja.
- Kila mara hakikisha kuwa mazoezi kwa vitendo na wateja yanafanyika kwa usalama
- Andika kwenye fomu kama mshiriki wa mafunzo ameweza kuonyesha kila stadi kwa usahihi. Toa maelezo zaidi kwa umia sehemu ya kutoa maoni. Inawezekana ikawa mambo yanayofanyika vizuri, maeneo ambayo yanastahili kufanyiwa mazoezi zaidi.

**Toa mrejesho kwa washiriki wa mafunzo:**

- Jadili pamoja na washiriki wa mafunzo kuhusu mambo uliyoweza kuyaona. Waambie kuhusu uwezo wao, na maeneo ambayo wanahitaji kufany amazoezi zaidi.
- Mpe mshiriki wa mafunzo nakala ya orodha iliyokamilika, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu.
- Endelea kuwashauri na kuwasaidia na kuwafanyia tathmini kwa mara nyingine kwa kadri wanavyoongeza stadi na hali ya kujiamini.

**Je, ni wakati gani mshiriki wa mafunzo, anaweza kugawa vioo kuza na darubini bila ya kuwa na msaada?**

- Ili kuwa na uwezo wa kugawa vioo kuza na darubini kwa usalama, mshiriki wa mafunzo anapaswa kutekeleza stadi zote kwa usahihi.
- Kumbuka: Kutoa ushauri na kusimamia ni mchakato endelevu, ili kuboresha stadi.